

Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia

Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Unyanyasaji wa Kijinsia Mwaka 2016

Mwongozo wa Majadiliano kwa Njia ya Bango



Building Momentum • Fostering Activism

Vunja ukimya, Ondoa Vikwazo! Unawezaje kufanya Elimu Kuwa Salama kwa Wasichana?

Bango ni nyenzo yenye nguvu katika mawasiliano. Hii ni kwa sababu linaweza kutumika kwa watu mbalimbali bila ya kujali viwango vyao vya elimu. Kama nyenzo muhimu ya mawasiliano katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake bango pia linaweza kutumika kama chombo kinachoweza kushiriki jamii. Kabla ya kuonyesha bango unaweza kushirikisha vikundi vidogo vya watu katika mijadala kuhusiana na kauli mbiu iliyopo katika bango. Tumia maswali yafuatayo hapo chini katika kuongoza majadiliano yako yatokanayo na kauli mbiu ya mwaka huu inayo elezea vikwazo wanavyokabiliana navyo wasichana katika kupata elimu.

Dondoo za Majadiliano kwa Njia ya Bango

1. Majadiliano ya kikundi yanatakiwa kuwa na watu wasiozidi 15 ili yaweze kufanyika kwa ufanisi. Yanaweza kufanyika katika mazingira yoyote ndani ya jamii ambapo watu wanaweza kukusanyika na kufanya majadiliano, kwa mfano, chini ya mti, nje ya nyumba ya mtu, katika saluni, katika bar, nk
2. Waeleze washiriki kwamba hakuna majibu sahihi au yasiyo sahihi. Washukuru washiriki kwa michango ya mawazo yote waliotoa.
3. Kumbuka kwamba maswali haya ni mwongozo tu katika majadiliano. Hakuna haja ya kusoma maswali kama yalivyoandikwa au kufuata jinsi yalivyopangiliwa. Jaribu kuyafanya majadiliano yawe ya kawaida na uliza maswali ya uchokozi ili kuibua mjadala zaidi pale inapobidi.
4. Jaribu kuhimiza uchangiaji kutoka kwa washiriki wote, na kuwapa fursa sawa ya kushiriki.
5. Kumbuka usiwaelekeze washiriki mambo ya kufikiria. Kuuliza maswali inaweza kuwa njia bora zaidi kuliko kutoa ujumbe.
6. Baada ya kukamilisha majadiliano, bandika bango katika eneo lililo wazi ili washiriki wa kundi hilo waweze kuliona.

Mapendekezo ya Maswali ya Majadiliano

1. Je, unaona nini katika bango? Je unapata ujumbe gani kutoka katika bango hili?
2. Ni jinsi gani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana unachangia kiwango cha chini cha uandikishwaji na kuendelea kuwepo shuleni?
3. Ni vikwazo gani kwenye kaya zetu vinavyoathiri upatikanaji wa elimu kwa wasichana ?
4. Ni vikwazo gani wasichana wanavyokabiliana navyo njiani wanapokwenda shuleni vinavyo athiri upatikanaji wa elimu?
5. Ni vikwazo gani katika shule zetu vinavyoathiri upatikanaji wa elimu kwa wasichana?
6. Ni vikwazo gani katika sera zetu za elimu kwa ujumla na mitaala vinavyoathiri upatikanaji wa elimu kwa wasichana ?
7. Je, kuna faida gani wasichana wengi kupata fursa ya elimu na kumaliza masomo yao? (Kwa mtu binafsi, ngazi ya kaya, na jamii kwa ujumla)
8. Ni hatua gani unaweza kuchukua kama mtu binafsi kuondoa vikwazo vya elimu kwa wasichana?